**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| MHE. ZUBEIR ALI MAULID | - | SPIKA |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera |
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 35. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 37. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 38. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |
| 41. Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Nafasi za Wanawake |
| 42. Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Shaurimoyo |
| 43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |

44. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

**Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 28 Februari, 2018**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 56**

**Makusanyo ya Fedha kwa Wizara**

**Mhe. Omar Seif Abeid -** Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilijipangia kukusanya Tshs. 487,400,000/= lakini hadi kumaliza kwa kipindi hicho, Wizara haikukamilisha lengo la makusanyo hayo. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imejipangia kukusanya jumla ya Tshs. 891,078,000/= ambapo ni sawa na ongezeko la Tshs. 403,678,000/=.

(a) Je, hadi kufikia mwezi Disemba, 2017 Wizara kupitia taasisi zake imeshakusanya kiasi gani cha fedha kwenye malengo yake iliyojipangia.

(b) Je, hadi kufikia mwezi Disemba, 2017 ni mikataba mingapi ya ajira za nje, vibali vya kazi kwa wageni vimetolewa, na ni vyama vingapi vya ushirika ambavyo vimesajiliwa.

(c) Je, hadi sasa ni upi mwelekeo wa Wizara hiyo kuhusu kufikia lengo la makusanyo ambayo Wizara kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2018 umejipangia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto** - Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ameweza kutupa pumzi zake na tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wenye afya njema.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara kufikia mwezi wa Disemba, 2017 kupitia taasisi zake imeshakusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne na Moja, Laki Saba Sitini Saba Elfu Mia Saba na Hamsini (401,767,750/=) sawa na asilimia 45 ya lengo lililojiwekea kwa mwaka. Kati ya fedha hizo Shilingi Mia Tatu Arobaini na Tatu Laki Nne Arobaini na Saba Elfu Mia Saba na Hamsini (343,447,750) zimetokana na vibali vya kazi kwa wageni, Shilingi Milioni Ishirini na Laki Moja (20,100,000/=) kutokana na mikataba ya ajira za nje. Shilingi Milioni Sita Tisini na Tano Elfu (6,095,000/=) zilikusanywa kutokana na

ada za usajili na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Shilingi Milioni Saba na Laki Sita (7,600,000/=) zimekusanywa kutokana na ada ya ukodishaji wa ukumbi.

(b) Mhe. Spika, kwa upande wa ajira za nje ya nchi hadi kufikia Disemba, 2017 jumla ya vijana 220 walinufaika na ajira hizo. Hadi kufikia Disemba, 2017 vibali vya kazi 942 kwa wageni vimetolewa, na jumla ya Vyama vya Ushirika 144 vimesajiliwa.

(c) Mhe. Spika, mwelekeo wa wizara katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2018 ni kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha ufuatiliaji wa Maofisa Wakaguzi katika maeneo ya kazi na Vyama vya Ushirika ambapo hadi kufikia Disemba, 2017 tayari Wizara imekaribia kufikia nusu ya lengo la makusanyo yaliyopangwa kwa mwaka asilimia 45.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, nachukua fursa hii kuipongeza sana wizara kwa bidii yake ya kuendeleza mwelekeo mzuri wa makusanyo ya kodi. Lakini nilitaka nijue tu kutokana na huo mwelekeo mzuri ambao umejionesha hadi hivi sasa, pengine ni kitu gani kilichochangia kuongezeka kwa mapato hayo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Sababu iliyopelekea kuongezeka kwa mapato hayo ni kuongezeka kwa vibali kutoka nje, hiyo ndio sababu iliyosababisha mapato kuongezeka kutokana na vibali vya ajira za nje.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, napenda nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake mama alitueleza kwamba makusanyo yamefikia asilimia 45 sawa na nusu ya makadirio ya bajeti ambayo amepanga mwaka 2017/2018. Hapa bado asilimia nyingi kufikia yale malengo yaani asilimia 100. Kwa hivyo, nilitaka kuuliza tu kwa mwaka 2017/2018 wizara ilijipangia kukusanya jumla ya shilingi ngapi na hatimaye kwa sasa imefikia kukusanya asilimia 45.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa swali la Mhe. Mwakilishi linahitaji takwimu sahihi za fedha. Kwa hivyo, naomba swali lake hili niweze kumjibu kwa maandishi.

**Nam. 60**

**Matayarisho ya Mashindano ya Michezo**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa asubuhi njema, awali ya yote napenda muungane na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na tumtakie kheri Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*). Mhe. Spika, naomba kujibiwa swali langu Nam. 60.

Pamoja na jitihada za serikali kuendeleza michezo ya aina zote na kuleta mafanikio kama tulivyofanikiwa katika mashindano ya *CECAFA*, yapo baadhi ya mambo ambayo tunatakiwa kujipanga ili kuleta mafanikio zaidi.

(a) Je, serikali imejipangaje kwa wanamichezo kuwapima afya zao na uwekaji wa kambi za mazoezi ya kimashindano.

(b) Kuna matamasha mengi yanayofanyika Zanzibar kama Tamasha la Nchi za Jahazi na mengineyo, lakini matamasha haya sijawahi kuona kilele kikafanyika Pemba kwa nini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa wizara yangu inapokea pongezi kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za kuendeleza michezo ya aina zote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kupitia nia ile ile ya kujipanga vyema katika mashindano ya kila aina kama ilivyooneshwa katika mashindano ya *CECAFA* na kulitambulisha jina la Zanzibar kuwa ni moja ya nchi inayotoa wanamichezo walio bora na wenye uwezo.

a) Mhe. Spika, serikali katika kuhakikisha inatoa wanamichezo walio bora, pamoja na maandalizi mengine itafanya juhudi za makusudi kwa wanamichezo kuwapima afya zao ikiwemo kuhakikisha hawatumii madawa ya kusisimua misuli na kuongeza nguvu michezoni kwenye maandalizi ya kambi za mazoezi kwa ajili ya mashindano ya Kimataifa.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa matamasha mengi yanafanyika Unguja kama Tamasha la Nchi za Jahazi na mengineyo ambapo kilele chake hakijaonekana kufanyika Pemba.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nimuongezee tu lenye kifungu (a) na (b). Kwa kuwa Unguja tayari inajulikana kwa mambo ya utalii na watalii wakitoka katika maeneo yao wanaita Zanzibar, na Zanzibar kwa mambo ya nchi ni Unguja na Pemba, lakini kwa mambo ya kikawaida ni Zanzibar ndio Unguja. Hata ukiwa katika ndege unaambiwa tunatua katika Uwanja wa *Karume International* ulioko Zanzibar, sio ulioko Unguja ni ulioko Zanzibar.

(a) Je, kwa kuwa tayari kisiwa cha Unguja tayari kimeshaweka mwelekeo katika utalii na kisiwa cha Pemba ndio kwanza *fresh* hakijajulikana katika utalii wake. Je, utafanya juhudi gani za kuweza kuwapeleka kwa makusudi watalii, ili kuweza kukitangaza kisiwa cha Pemba.

(b) Kwa kuwa wachezaji wanaocheza timu za taifa, wanakuwa wengi wanachezea timu kubwa zilizoko katika daraja kubwa katika nchi nyengine na wanapotakiwa na nchi zao, wakiitwa katika timu ya taifa wako *fresh*, wako kimazoezi na wako ki-*format.* Lakini

wachezaji wetu wengi walioko katika timu ya *Zanzibar Heroes* wanakuwa ni wachezaji baadhi ya timu ndogo ndogo, wachezaji hawa sasa hivi wametawanyika.

Je, umejipanga vipi kuwawekea kambi wachezaji hawa wakati wa karibu na mashindano.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) vyote kwa pamoja kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, juhudi ambazo nitazifanya kwa upande wa kisiwa cha Pemba kuwapeleka watalii katika kisiwa kile, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi hii ipo na ni endelevu na kwa upande wa Pemba tunazo hoteli mbali mbali.

Mhe. Spika, pia kuna maeneo sasa hivi tumeyatenga kwa ajili ya kujenga mahoteli. Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tutafanya juhudi ya kuwapeleka watalii kule ili nao wao wakajionee mazingira ya kisiwa cha Pemba.

(b) Mhe. Spika, mipango ambayo tunajipangia ya kuwachukua wachezaji wale *Zanzibar Heroes* ambao sasa hivi wamo katika vilabu mbali mbali ambavyo vimewachukua kwa ajili ya kukuza vipaji vyao, pia kwa ajili ya kuonesha vipaji vyao vizuri. Kwa kuwa nimesema katika swali langu mama kwamba sisi tuna vipaji vizuri na wachezaji walio bora wakati utakapofika karibu na mashindano haya, tutahakikisha kwamba wachezaji hawa tumewachukua wote na kuwaweka pamoja kwa ajili ya kufanya mazoezi ya mashindano ya timu yetu ya *Zanzibar Heroes.*

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vipengele (a) na (b). Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu swali lake alisema kwamba kwa kupitia *spirit* ile ile ya kujipanga vyema katika mashindano ya aina mbali mbali na kuitangaza vyema Zanzibar katika nyanja za ulimwengu.

Je, kwa kuwa Zanzibar mara ya mwisho kuandaa mashindano ya kimataifa, wakati ule akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Haroun Ali Suleiman na Zanzibar kuweza kuchukua ubingwa wa *under nineteen* tokea kipindi kile hatujaandaa tena mashindano.

Je, tunajipanga lini tena ili kuandaa mashindano ya *Club* Bingwa yanayoandaliwa na *CECAFA* au *Challenge Cup*, hata kuandaa mashindano yanayoshirikisha Klabu Bingwa ya Afrika. Kwa sababu Mhe. Spika, Zanzibar ni mwanachama wa *CAF* Chama cha Mpira wa Miguu Afrika. Kwa sababu mashindano yale ya Klabu Bingwa ya Afrika huandaliwa nchi mbali mbali. Je, Zanzibar tunajipanga vipi ili kuwa wanachama au tunaandaa mashindano haya ya Afrika, ikiwa sisi ni wanachama wa *CAF*.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba naungana na yeye kwamba sisi tunahitajika kuandaa michezo hii ambayo wenzetu wanaandaa mashindano haya.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba tutashauriana na zile nchi ambazo tumo katika uanachama au nchi ambazo wanaandaa mashindano haya, ili wakati itakapofika zamu yetu na sisi tutayaandaa na mashindano yetu yatakuja kuchezwa hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe Naibu Waziri, nataka kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, ubora wa kitu unahitaji mipango bora na madhubuti. Nataka kuuliza kwamba katika suala la kukuza vipaji wizara yako imejipanga kuwa na eneo la ujenzi wa kituo cha kukuza vipaji kama kile cha Jakaya Kikwete kilichopo Dar es Salaam. Kama mnalo, ni lini mipango hiyo ya ujenzi itaanza.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kwamba dhamira ya kujenga viwanja hivi vya vipaji tunayo, lakini wakati sasa hivi tumo katika utaratibu wa kujenga viwanja hivi kikiwemo cha Mao Tse Tung na tunatarajia tujenge viwanja vyengine. Kwa hivyo, ndani ya viwanja hivi kutakuwemo na sehemu mbali mbali za michezo, ikiwemo pia ya kuonesha vipaji vya wananchi wetu au vijana wetu ambao wamo hapa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii

**Mhe. Spika:** Samahani Mhe. Suleiman Makame. Mhe. Ali Salum Haji.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, samahani Mhe. Naibu Waziri kajitahidi, lakini na Mhe. Waziri alikuwa anataka kusimama. Lengo lilikuwa sio viwanja, ni jengo maalum litakalowekwa kutayarisha ukuzaji wa vipaji na nikatoa mfano kama la Jakaya Kikwete lile la Dar es Salaam kama kituo yaani *centre* maalum.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika. kwanza kabisa napenda nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kuendelea kujibu maswali kwa ufasaha kabisa. Lakini napenda nichukue fursa hii kumuongezea Mhe. Ali Salum Haji Mnadhim majibu katika swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna umuhimu kuwa na mipango ya kuendeleza vipaji katika *academy* maalum na Zanzibar haiko nyuma katika hilo.

Mhe. Spika, kama anavyokumbuka au watakavyokumbuka wengi kwamba tunayo *centre* pale tumeianzisha na hivi sasa imo katika mipango ya kuendelezwa ambayo ipo katika Kituo cha Dole, kwa jina inaitwa *DATH,* yaani *Dole Academy of Both.* Kwa hivyo, dhamira kama zile alizokuwa nazo Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete Zanzibar ilizianzisha mwanzo na wenzetu walikuja kufuatia yale ambayo sisi tumeyadhamiria kuyafanya. Lakini kama alivyosema michezo ni gharama na kutengeneza vituo vile ni gharama, hivi sasa tumekuwa tunapokea maombi mengi ya watu ambao wanataka kufanya vituo vile.

Mhe. Spika, nataka nimuarifu tu tayari kwamba wiki iliyopita tumepokea ujumbe kutoka Ujerumani wapo tayari kuanzisha *academy*. Lakini kocha wetu Mr. Moroko tayari katika sehemu alizoitwa kwenda kufundisha timu mbali mbali na yeye tayari ameahidiwa kujenga *academy*

yake na sasa hivi tumo katika taarifa za kutafuta kiwanja ili tuwe na *academy* zetu za kukuza vipaji hapa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yako umesema kwamba kunafanyika matamasha.

a) Je, Mhe. Waziri ndani ya mwaka 2016 mpaka hapa tulipo mwaka 2018 ni matamasha mangapi yamefanyika Pemba na ni matamasha ya aina gani.

b) Umesema kuna maeneo Pemba mmetenga kwa ajili ya kujenga mahoteli katika jimbo langu. Kuna fukwe nzuri na hadi leo kuna *beacon* tu zimechomekwa. Je, ni maeneo gani yaliyotengwa kujengwa mahoteli hayo na ni hoteli za aina gani mtakazozijenga huko Pemba.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamadni na Michezo naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Mwakilishi ametaka kujua ni idadi ya matamasha mangapi ambayo tumeyafanya kuanzia mwaka 2016 hadi kufikia leo. Swali hili naomba nilifanyie utafiti kwa kina na baadae nitamjibu kwa maandishi. Ahsante Mhe. Spika.

**Nam. 67**

**Mipango ya Serikali kuweka Maeneo ya Viwanja vya Michezo**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:-

Mafanikio ya timu ya Zanzibar iliyoyapata katika mashindano ya *CECAFA* pamoja na kitendo cha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwatunukia zawadi wachezaji hao, imeleta hamasa kubwa kwa vijana wetu kupenda michezo.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuwawekea watoto maeneo ya kuchezea mipira katika maeneo ya Miji Mikongwe na Miji Mipya.

(b) Je, yako wapi maeneo ya viwanja katika miji ya *plan* kama Mombasa kwa Mchina, Mpendae, Chukwani na maeneo kama hayo.

(c) Je, suala la viwanja vya michezo katika maeneo kama hayo hayakuzingatiwa na kama yalizingatiwa yako wapi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 67 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali kupitia Sera ya Michezo imejipanga kuwawekea watoto maeneo ya kuchezea mpira katika maeneo ya miji mipya na miji mikongwe. Ndani ya sera hii imezingatiwa suala la kuzuia uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa michezo (viwanja vipya na vikongwe).

(b) Katika miji mipya ambayo imejengwa kwa *plan* kama Mombasa kwa Mchina, Mpendae, Chukwani na maeneo kama hayo, Idara ya Mipango Miji na Vijiji ilitenga maeneo ya kufanya shughuli za jamii na michezo. Mengi ya maeneo hayo kwa sasa yamevamiwa kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za makaazi na baadhi bado yanaendelea kutumika kwa shughuli za kijamii na michezo kwa watoto.

(c) Suala la uvamizi wa viwanja vya michezo katika maeneo yaliyotajwa hapo juu yamezingatiwa katika kiwango kidogo na hivi sasa wanamichezo wanatumia viwanja vya Magereza pembezoni baina ya barabara na nyumba za Mchina.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

**Mhe. Spika:** Hapana Mheshimiwa.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi nimshukuru Mhe.Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimuulize Waziri kwamba ameniambia katika jibu lake kuna viwanja vimepimwa au mipango miji ilipima viwanja na viwanja hivi tayari vimeshajengwa nyumba. Lakini ramani ya nyumba hizi na viwanja hivi vipo na nia ya serikali ni kuhakikisha wanamichezo wanapata sehemu zao na watoto pahala pa kuchezea. Kwa mfano mdogo tu hivi karibuni Rais John Pombe Magufuli alivunja Juma la *TANESCO* kwa kupitisha barabara. Je, Waziri ananambiaje nyumba zilizovamia viwanja atazifanya vipi au ndio tumeliwa.

Mhe. Spika, la pili Mhe. Waziri amesema katika swali (c) majibu yake kama vijana wanacheza mpira katika maeneo ya Viwanja vya Magereza na pembezoni mwa barabara ya kwa Mchina kama tuna lengo la kujipanga la kuweza michezo kiwango cha kimataifa. Je, pembezoni mwa barabara unaweza kucheza mipira.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hatua ambazo tutazichukua kwa wale watu ambao wamevamia viwanja hivi, kwanza kabisa tutahakikisha kwamba viwanja vile vyote ambavyo vimevamiwa tutashirikiana na mamlaka husika, kwa mfano Wizara ya Ardhi, Maji,Nishati na Mazingira. Lakini pia na kwa wale ambao wamepewa viwanja hivi kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambao wanayo maeneo katika skuli zao ili kudhibiti viwanja hivi. Lakini na kwa upande wa ujenzi wale ambao tayari wameshajenga tutashirikiana na watu wa mipango miji kuhakikisha kwamba watu wale sheria imefuata mkondo wake na kuondosha kwa ajili ya kuondoa uvamizi ule.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba pembezoni mwa barabara na sio barabarani kwa hiyo kwa maana ya pembezoni, pembezoni ni sawa sawa na kusema ni pembeni mwa barabara. Kwa hiyo, haimaanishi kwamba vijana wetu wasiweze kucheza mpira kwa sababu ipo karibu. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kupata fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana kwa majibu mazuri na maelezo marefu ya swali lake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukweli kwamba viwanja vyetu vya michezo vingi kama Mnazi Mmoja, Maisara, Sebleni, Gombani ya Kale, vimechoka tena baada ya kuwa majani kuna mchanga hasa, sasa vijana wetu wanapata tabu kufanya mazoezi inavyopaswa, ule mpira hasa haukai chini. Sasa Wizara yake Mhe. Waziri ina mpango gani wa kupanda majani na kuvitunza kuviendeleza viwanja vile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tunajua kwamba viwanja vyote vya michezo vipo chini ya Wizara Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba tutashirikiana na wadau ambao wanavitumia viwanja vile na kuwashauri tupande majani ambayo yatahakikisha yameondosha mchanga ule ambao vijana wetu au wanamichezo wetu ni vikwazo kwa ajili ya kufanya mazoezi ambayo wanayafanya siku hadi siku. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kuhusiana na michezo, hivi karibuni tumepata habari njema kwamba Zanzibar imeanza kuuza wachezaji na mchezaji Selembe amenunuliwa.

Je, wizara imeandaa utaratibu gani wa kibajeti kulea vipaji, ili *agency* zile zitakapokuja ziwe na kituo cha kufikia na serikali inaunganishwa baina ya *agency*, *academic* na wanunuzi wa mchezaji. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana anayoendelea kujibu Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli Zanzibar tumeanza kupata ma-*agent* wa kununua wachezaji. Mwezi mmoja uliopita Mhe. Spika, nilipata *agent* kutoka vilabu vya daraja la kwanza vya Uingereza ambao kwa nia nzuri kabisa wamewataka wachezaji wetu wa timu ya taifa akiwemo Toto Fey.

Mhe. Spika, Zanzibar ina chama chake cha mpira yaani *Zanzibar Football Association* (*ZFA*) na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina dhamira za dhati kabisa kufanya marekebisho makubwa ndani ya chama hiki cha *ZFA*. Ndani ya *reform* hizo naamini wazi kutakuwa na taratibu za kuweza kupokea ma-*agent* na kuweza kukaa na ma-*agent* na kuwa na ma- *agent* wa nyumbani ambao wanaweza kuuza wachezaji wetu nje ya nchi. Nashukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Machano Othman Said:** Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika suala la msingi lilizungumziwa viwanja na kama tunavyoelewa wiki iliyopita familia ya soka Tanzania ilimpokea Rais wa *FIFA* Florontine na katika watu waliokwenda katika mapokezi hayo ni Waziri wetu wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Katika mazungumzo na Waziri Mkuu na *TFA*, *FIFA* imeahidi kujenga viwanja 9 Tanzania. Je, Zanzibar katika 9 hivi tunapata vingapi na katika 9 hivyo kama vipo vya Zanzibar vitajengwa katika eneo gani.

(b) Bara baada ya kuondoka Rais wa *FIFA* imetumbukiza fedha bilioni 2 kwa *TFA*. Je, Zanzibar tunapata angalau gawio lolote katika fedha hizo.

(c) Kwa muda mrefu kiasi miaka 20 hadi 25 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifikiria *ZFA* kupokea udhamini kwa makampuni yaliyotaka kudhamini Ligi ya Zanzibar lakini yana viashiria vya biashara ya pombe. Lakini hadi muda huu ni miaka 20 – 25 timu za Zanzibar zinacheza ligi wachezaji wanapewa shs. 200 na refa shs. 300. Ni lini serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kwa makusudi kuwasaidia *ZFA* wapate udhamini wa ligi ili timu zetu ziwe bora na ziweze kutoa ushindani mkubwa na kutoa timu bora ya Taifa. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza lenye vipengele vitatu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba mimi mwenyewe nilikuja kukuaga nikaomba ruhusa pamoja na kuweza kuhimili kuja kwenye Baraza lako wakati wa asubuhi lakini usiku wa saa 10:00 tulimpokea Rais wa Shirikisho la Mpira la Dunia *(FIFA)* Florontine na katika kumpokea kule alipata bashasha sana kuona kwamba serikali zote mbili zimekwenda na zimempokea. Amepata elimu zaidi kujua kwamba suala la michezo ndani ya Zanzibar na Tanzania, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala linaloshughulikiwa kwa serikali mbili tofauti kwa jitihada kubwa za Mhe. Waziri Mkuu.

Niendelee kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli katika ujumbe wake kwa Rais Florontine ni kumuagizia kutusaidia viwanja ndani ya zoni 9 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya viwanja vile 7 vitajengwa Tanzania Bara na 2 vitajengwa Zanzibar. Rais Florontine amekuwa ana muelekeo wa makubaliano na hilo amelipokea na amelikubali kwa vizuri. Nataka nikuthibitishie kwamba viwanja vitakavyojengwa Zanzibar, Mhe. Magufuli amevieleza kwa machungu yake kabisa kwamba kimoja kitajengwa Zanzibar yaani Unguja na kimoja kitajengwa Zanzibar yaani upande wa Pemba. Kwa hivyo, viwanja hivyo vitakuwa na magao wa aina hiyo. *(Makofi)*

(b) Kuhusu fedha ambazo Mhe. Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu la Dunia aliziingiza aliweza kupata motisha kwa namna alivyopokewa na kuongeza fedha kutoka Dola Laki Mbili na Nusu ($250,000) ambazo zilikuwa zinapatikana kwa *TFF* kwa mwaka, hivi sasa ameongeza Dola Milioni Moja Laki Mbili na Hamsini ($ 1,250,000) ni faraja kubwa sana.

*TFF* yenyewe imeahidi kutoa sehemu ya pesa kuweza kuipa Zanzibar na ndio maana nikasema *ZFA* lazima ipite katika *reform* na Wizara itahakikisha kwamba itafanya *reform* kwa *ZFA*, ili tupate chombo ambacho kinaweza kusimamia vipaji vyetu vya maumbile kabisa. Lakini ndani ya mgao huo Rais Florontine aliahidi kwamba Dola Laki Moja ($100,000) ianze kupewa *ZFA* ili kuweza kutengenezea masuala yake katika mgao huu unaotolewa wa $250,000. Zitakapofika hizo fedha nyengine bila shaka mgao huo utakuwa na maendeleo zaidi. Muhimu ya hilo fedha zitumike kwa kuendeleza soka la vijana, soka la wanawake na soka la *beach*. Kwa hivyo, zitakuwa na matumizi maalum. Cha kupendezesha zaidi na Rais wa *CAF* ambaye walifuatana na Rais wa *FIFA* na yeye aliweka mgao wa Dola Laki Moja ($100,000) kuzipatia *ZFA*, kwa hivyo ziara ile ina manufaa makubwa kwa upande wetu.

(c) Kuhusu suala la udhamini nataka nimthibitishie kwamba wizara imekuwa na juhudi imeweza kwanza kufanya mazungumzo na wazelendo wa nchi hii na wapo wenye ari na tayari wamekuwa na muelekeo mkubwa sana. Tumezungumza na kampuni ya *Bakhresa Group* kama alivyoonesha ari ya kuweza kusaidia Kombe la Mapinduzi na akaweza kutusaidia milioni 55,000/= katika kuendeleza kombe lile. Udhamini upo na udhamini wa ligi yetu utakuwa ni endelevu katika kipindi kifupi, niwaombe tu watu kama Mhe. Miraji Khamis Mussa, Marais wa timu za *African Coast* wanaweza kuendeleza soka vizuri ili wasishuke daraja. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 52**

**Ujio wa Madaktari kutoka India**

**Mhe. Omar Seif Abeid -** Aliuliza:-

Kwa kuwa madaktari kutoka Hospitali ya Miot ya nchini India ambayo ndipo tunapopeleka wagonjwa wetu wengi kwa matibabu mbali mbali walikuja hapa nchini kwa ajili ya kutoa huduma za kutibu wagonjwa. Kwa kuwa kabla ya ujio wao kulikuwa na wagonjwa ambao walipaswa kupelekwa huko India kwa ajili ya matibabu.

a) Je, ujio wa madaktari hao wameokoa kiasi gani cha fedha ambacho kingetumika kwa kupeleka wagonjwa wetu huko.

b) Je, madaktari hao waliweza kuhudumia wagonjwa wangapi.

c) Je, madaktari hao waliwatibu maradhi gani.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu sana leo kwa kikao hichi kuwa ni mtu wa mwisho kufunga maswali. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii maana nimefunga maswali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 52 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naomba nichukue fursa hii kuwashukuru madaktari kutoka Hospitali ya Miot nchini India kwa imani yao na upendo kwa wananchi wa Zanzibar, ambapo kwa mara ya mwisho walifika Zanzibar mwezi wa Disemba, 2017 kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wetu 390, ambao walikuwa na maradhi mbali mbali pamoja wale waliokwenda India kwa matibabu. Pia waliwaona wagonjwa ambao ni mara ya kwanza na kuwashughulikia wagonjwa ambao walikwishapata matibabu kabla kwa ajili ya ufuatiliaji wa tiba zao.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kiasi gani cha fedha kingetumika kwa kuwapeleka wagonjwa hao India naomba kujibu swali hili kwa uhaba wake na sio ukamilifu kutokana na mazingira ya swali lenyewe lilivyo.

Mhe. Spika, kutokana na kuwa wapo wagonjwa ambao tunawasafirisha kwenda India wakifuatana na jamaa zao, na wapo wagonjwa ambao tunawasafirisha wakifuatana na madaktari wetu, na mara nyingi daktari mmoja huyo hufuatana na wagonjwa zaidi ya mmoja. Hivyo, jumla ya shilingi za Kitanzania 468,000,000/- (millioni mia nne na sitini na nane elfu) zingetumika kwa kusafirisha wagonjwa hao na shilingi za Kitanzania 585,000,000/- (millioni mia tano na thamanini na tano na thamanini na tano elfu) zingetumika kwa matibabu.

Mhe. Spika, hesabu hii ya matibabu, tumeichukulia ya bei au kiwango cha chini cha matibabu, kwani gharama za matibabu kule hutegemea na maradhi ya mgonjwa au ukubwa wa tatizo lenyewe. Ahsante.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi sina budi kurudisha shukrani zangu kwa madaktari hao kutoka Hospitali ya Miot ambao wameonesha upendo mkubwa kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Kwa sababu tukiangalia kwa haraka haraka ni karibu shilingi bilioni 1,053,000,000/= ambazo wametusaidia zingetumika. Kwa hiyo, hatuna budi na sisi kuwapongeza, lakini pamoja na hayo ningelitaka kujua.

a) Je, kuna utaratibu wowote utakaotumika au uliotumika wa kuwapeleka madaktari hao kutoka Hospitali ya Miot kwenda kutoa huduma kama hizo kule Pemba badala ya kuwaweka tu hapa na kuwaacha hapa Mnazi Mmoja.

b) Kwa kuwa maradhi ya moyo ni miongoni mwa maradhi yanayowasumbua sana wananchi wetu wa Zanzibar na ikitiliwa maanani kwamba wananchi wetu ni maskini. Swali langu, hapa imeonekana kama wametibu maradhi hayo ya uti wa mgongo hawakugusa mambo ya moyo. Je, kuna utaratibu gani wa madaktari hawa watakapokuja tukawapata kwa ajili ya kutoa huduma za maradhi ya moyo ambayo ni thakili hapa kwetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, tunao mpango wa kuwapeleka katika hospitali za Pemba pia kutoa matibabu lakini usiwe na wasi wasi na matibabu waliyoyatoa. Wananchi au wagonjwa kutoka Pemba walipatiwa matibabu kwa idadi kubwa, baada ya kutoka matangazo wagonjwa mbali mbali waliofika na wagonjwa kutoka Pemba walijitokeza na walitibiwa pamoja na

wagonjwa wenzao kutoka Unguja bila ya ubaguzi wowote. Hata hivyo, tuna mpango wakija mara nyengine kuwashauri sio kuwalazimisha wakipenda tutawapeleka waende wakatoe huduma katika hospitali zetu za Pemba.

b) Kuhusu swali (b) naomba kidogo Mjumbe arudie.

**Mhe. Spika:** Swali kuhusiana na matibabu ya moyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunikumbusha. Mhe. Spika, madaktari wetu hawa walivyokuja walitoa matibabu mbali mbali yakiwemo pia matibabu ya moyo ingawaje hapa sikueleza, lakini walijikita sana katika matibabu ya mgongo pamoja na mifupa, lakini matibabu ya moyo pia walitoa hususan kwa watoto wetu.

**Mhe. Hamida Abdalla Issa:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nilikuwa na swali dogo la nyongeza.

Pamoja na gharama ambazo serikali imenusuru kwa kuwaleta hawa madaktari kutoka katika hospitali ya Miot, lakini pia zipo gharama ambazo serikali imetumia kwa kuwafanyia matibabu wagonjwa hawa hapa hapa nchini. Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetumika katika kuwafanyia matibabu hapa hapa nchini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, gharama za matibabu ambazo tunatumia nchini kikawaida kuwatibu wagonjwa wetu ni nyingi na inawezekana inapita hata gharama ambazo tunatumia nje. Kwa sababu hizi gharama ambazo nimezitaja za nje ni gharama pengine zingechukua miezi mingi au miaka mitatu au minne. Sasa gharama za kuwatibu hapa hapa nchini ni nyingi na hapa sitoweza kukutajia kwa sababu inataka takwimu nikusanye mwezi fulani tumetumia gharama gani, lakini ukiangalia katika kitabu chetu cha bajeti jinsi tunavyoingiziwa pesa za bajeti ndio jinsi tunavyotumia kwa matibabu ya wagonjwa wetu.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi na mimi kuuliza suali la nyongeza. Kwanza niipongeze Wizara ya Afya hususan Waziri wa Afya, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa namna ya pekee anavyojitahidi kupambana kuona hali za wananchi wetu zinaimarika siku hadi siku. Juzi tu tulishuhudia madaktari kutoka Spain kuja kusaidia suala zima la operesheni wa masuala ya vichwa pale Mnazi Mmoja, tumeona jitihada zake binafsi Mhe. Waziri hongera sana katika hilo.

Je, madaktari wale waliweza kufanya operesheni ngapi pale ambazo zina thamani ya kiasi gani kuokoa fedha za nchi yetu kwa Zanzbar. Nathubutu kusema kwamba operesheni zile nje ya nchi kila moja sio chini ya dola elfu thalathini. Je, kwa Zanzibar operesheni ngapi juzi walifanya na zimeokoa kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, nishukuru kwa kunipa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuamsha wote wazima. Naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali yote yaliyoulizwa pamoja na ya nyongeza kwa ufasaha mkubwa sana. Naomba

tena nimshukuru Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa pongezi zake na kwa kuona jitihada zetu na naamini wajumbe wengine wengi watamuunga mkono katika hilo baada ya kuona jitihada zetu tunakwenda nazo kwa hali tuliyokuwa nayo na kwa hali halisi pia ya fedha tulizokuwa nazo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kweli tokea hawa ndugu zetu wa Spain kuingia nao mkataba ambayo tumefungua taasisi inayojulikana kwa jina la Miot, *Neuro Surgical Educational Development Unit of Zanzibar*. Mhe. Spika, hii Miot naomba niseme kwamba sasa hivi imeshapata cheti cha kutambulika Afrika ya Mashariki na Kati, kama kituo chenye ubora na kituo ambacho kinatoa elimu ya uti wa mgongo, mishipa ya fahamu, saratani ya ubongo, na masuala mengine yote yanayohusiana na mishipa ya fahamu.

Kwa hivyo, cheti hiki tulipokea mnamo mwezi wa Disemba mwaka jana, tokea waanze hawa ndugu zetu wa Spain kushirikiana na sisi wameshachukua vijana wetu saba kwenda nchini Spain kujifunza na vijana hao tayari wengine wamesharudi ambao wanaendelea kufanya kazi nao. Hivi karibuni tu tumetimiza jumla ya operesheni 1,200, hizi ni operesheni za uti wa mgongo, vichwa maji, mishipa ya fahamu, pamoja na saratani tano za kwenye ubongo, kati kati ya ubongo. Operesheni hizi hasa za saratani ya ubongo zimefanyika kwa mara ya kwanza Zanzibar na hizi tano ndio za kwanza hapa Zanzibar, kabla ya hapo tulikuwa tunapeleka wagonjwa hao nje ya nchi.

Nikichukua saratani hizi tano tu za ubongo basi ni zaidi ya dola moja na nusu ambazo ni sawa sawa na milioni mia tatu. Nikichukua wagonjwa wote kwa jumla Zanzibar basi katika miaka hii minne tokea wameanza tumeokoa zaidi ya dola milioni ishirini ambazo tungekuwa nazo zingetumika kuwapeleka wagonjwa ama wagonjwa wetu wangeathirika moja kwa moja. Kwa hivyo, taasisi hii tunaendelea kushirikiana nayo na hivi karibuni utafanyika mkutano mkubwa ambao naamini wawakilishi wote na wananchi wataweza kuona kupitia vyombo vya habari utakapokuja uongozi wa taasisi hii kutoka Spain. Kwa hivyo, takriban dola milioni ishirini kwa miaka hiyo yote iliyopita tumeweza kuokoa, hapo sijachukulia gharama za usafiri wa ndege pamoja na wasindikizaji ambao wamekwenda na wagonjwa hao nje ya nchi. Mhe. Spika, naomba jibu hili litosheleze, ahsante.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi na nikaweza kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, nichukue fursa hii kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri kwa jitihada zao kubwa wanazozifanya ndani ya nchi yetu ili kuwapatia huduma za kiafya wananchi wetu.

Lakini ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kweli huwa tunasikia na tunaona wagonjwa wengi wanaandikiwa rufaa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda nje ya nchi aidha India au kwengineko. Lakini kama wanapata hizo rufaa tunakuwa tuajiuliza maswali je, tatizo ni madaktari au tatizo ni vifaa.

Kama tatizo ni vifaa. Je, hao madaktari ambao wanatoka huko kuja hapa nchini kwetu kwa ajili ya kuwafanyia matibabu hao wananchi hivi vifaa wanavipata wapi au wanakuja navyo.

Kama tatizo ni madaktari. Je, wizara inajisikiaje kuona kwamba wale madaktari wanapotoka kule kuja hapa wasiwaunganishe na vijana wetu ambao wana ujuzi na fani hizi wanaoziweza,

wakaweza kuwaunganisha nao kwenda kuzidi kusomea hizi nafasi au huu ujuzi, ili madaktari hao na sisi tukawapata hapa na vifaa hivyo tukawa navyo hapa hayo matibabu yakaendelea kufanyika.

**Mhe. Spika:** Naomba uulize swali Mheshimiwa.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Naam.

**Mhe. Spika:** Naomba uulize swali usihutubie.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Swali ndio hilo Mhe. Spika. Je, wizara ina utaratibu gani au inachukua jitihada gani ya kuleta hivyo vifaa au hao madaktari kwenda kuwasomesha huko.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kupata fursa hii. Naomba nimshukuru sana Mhe. Hidaya Ali Makame kwa swali lake zuri sana la nyongeza.

Mhe. Spika, swali hili sio yeye Mhe. Hidaya Ali Makame tu anayejiuliza, hata sisi wizarani huwa tunakaa na Idara ya Mipango wakati tunapanga tunatazama kile tulichokuwa nacho mkononi, tunatazama wagonjwa waliopo wote ama ile *trend* ya wagonjwa kwa mwaka, na tunatazama gharama pia za matibabu nchi za nje. Tunapata tabu sana wakati mwengine tukiwa na dola milioni mbili mfano ama milioni tatu unasema hizi nizitumbukize kwenye vifaa niwaache hawa wagonjwa wahangaike, ama wengine wamalizikie hapa hapa, ama niziingize kwa wagonjwa, niokoe wagonjwa kwanza vifaa nitaendelea kuhangaika kutafuta. Hilo ni tatizo ambalo tunalipata mara nyingi na serikali mara zote inaweka maslahi ya mwananchi wake kwanza. Kwa hivyo, nishukuru kwa upande wa serikali kwamba hilo limekuwa ndio jambo kuu kabisa la kumuangalia mwananchi kwanza.

Sasa bajeti ya vifaa inapopatikana basi tunaelekea kwenye vifaa. Sasa ninachokifanya na wenzetu hawa na jambo ambalo limeonekana linafanya kazi vizuri sana ni kwamba tunashirikiana. Kama hawa taasisi ya Miot kuna fungu ambalo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaingiza pale moja kwa moja, mfano lile jengo pale kulipia bili ya umeme, bili ya maji, pamoja na wafanyakazi wote waliokuwepo pale mishahara wanalipwa na SMZ. Naomba nimjulishe Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba wao mara nyingi wakija wanakuja na vifaa vyao kamili.

Lakini naomba nitamke wazi katika mwelekeo wetu wa serikali pamoja na *vision* ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein maradhi yote haya ambayo sasa hivi tunakwenda kutibu nje, basi *vision* yake yaani ule mwelekeo ambao ametupa sisi maradhi haya tuwe tunatibu hapa hapa Zanzibar. Katika ramani ya Hospitali ya Binguni inayotarajiwa kujengwa hospitali ya kisasa na kubwa kabisa, tayari Mhe. Rais ameshatuagiza suala la maradhi ya moyo liwepo, suala la maradhi ya saratani liwepo, suala la maradhi ya mifupa ambao wagonjwa wengine unawapeleka kwa sababu ya maradhi ya mifupa pia liwepo huko, suala la kubadilisha figo pia liwepo. Kwa hivyo, *specialty* zote tunatarajia Binguni itakapomalizika zitakuwepo na *investment* ya vifaa hivyo itapitia katika huo mkopo ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatiliana saini pamoja na *Kuwait Fund, BADEA* na *Saudi Fund.*

Kwa hivyo, naomba Mhe. Hidaya Ali Makame pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote watuvumilie wakati tunakwenda na program hii hapa tulipo leo sipo tulipokuwepo huko nyuma, hata hao wenzetu India na wengine miaka kumi na tano ishirini walikuwa kama hivi. Kwa hivyo, wamechukua muda kufikia mpaka hapa. Mimi naamini chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein muda wetu wa kufikia huko utakuwa mfupi sana, sasa hivi tiba ya saratani tunaitoa Hospitali ya Mnazi Mmoja, hapo kabla tulikuwa hatutoi tumeanza mwaka jana, wagonjwa wote wa saratani walikuwa wanakwenda *Ocean Road* Dar-es-Salaam sasa hivi suala la *chemotherapy* kwa kupitia *drip* tumeanza kutoa hapa, hatukuanza kutoa kwa mionzi, mionzi bado wanakwenda *Ocean Road* Dar-es-Salaam hatujafikia huko bado.

Suala la *dialysis* tulikuwa hatutoi kusafisha mafigo lakini sasa hivi tumeanza kutoa chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein na hilo alitusimamia yeye na vifaa hivyo kaleta yeye mwenyewe pale Wizara ya Afya ambapo sisi vijana wetu wamepata nafasi ya kwenda kusoma kuweza kufanya tiba hizo. Kwa hivyo, hatua kwa hatua tutafikia huko alikosema Mhe. Hidaya Ali Makame yote Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaweza kufanya hapa hapa. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ali Suleiman Ali naomba kukupa nafasi ya mwisho kabisa ya kuuliza swali la nyongeza.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na kuwa baadhi ya wajumbe wamenifilisi lakini nitakuwa na swali dogo la nyongeza kwa faida ya wananchi wetu. Tunaamini kwamba Tanzania Bara wenzetu wamepita hatua sana kwa kukusanya maradhi mbali mbali katika kitengo kimoja na kuondoa adha kwa wagonjwa mbali mbali kusafirishwa nje ili kupunguza matumizi ya serikali.

Je, kwa kuzingatia hili, wizara pamoja na majibu aliyojibu Mhe. Waziri kwa makusudi ina mpango gani wa kuweka chuo hapa Zanzibar wakaja wataalam wetu kuwasomesha wataalam wa hapa Zanzibar, ili kurahisisha na kuondokana na kutumika pesa nyingi kupeleka nje, pesa zile zikapungua kwa matumizi ya ndani.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kukushukuru kunipa fursa hii na kumshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri sana la nyongeza.

Katika jitihada hizo hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanzisha *Faculty of Medicine* kupitia katika chuo kikuu chetu cha *SUZA.* Katika jitihada hizo hizo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshakitoa Chuo cha Afya kilichokuwepo hapa Mbweni, sasa hivi imekuwa ni sehemu ya chuo kikuu cha *SUZA* sio tena kituo cha Wizara ya Afya au chuo cha Wizara ya Afya, lakini ni sehemu ya chuo kikuu cha *SUZA.* Kwa hivyo, katika jitihada hizo hizo tayari *SUZA* imeshatiliana mikataba na vyuo vikuu zaidi ya 10 kushirikiana nao kwenye taaluma mbali mbali, wale wa Cuba mliokuwa mnawaona wanakuja Hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa wanakuja *part time* lakini *full time* wanakwenda *SUZA* kusomesha vijana wetu, vijana mahiri, vijana waliopasi, vijana wazalendo ambao wanaosomea fani hizo.

Lakini hiyo isitoshe Mhe. Spika, Wachina nao pia tayari wameshajitokeza kufanya mafunzo pamoja na sisi kupitia *SUZA,* lakini *practical* zote watakuwa wanafanya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hivi karibuni tumeweza kukubaliana na hospitali tano India ambao nao pia wamekubali

kuleta walimu wao hapa kuja kutoa mafunzo hayo *SUZA*. Lakini wakati huo huo, wametupa *offer* ya vijana wetu zaidi ya saba kwenda India kuwasomesha, sisi tutalipia nauli pamoja na makaazi yao, lakini masomo yote watalipia wao. Kwa hivyo, idadi ya wataalam nashukuru inaendelea kuongezeka, haikupata kutokezea katika historia ya Zanzibar wataalam kuwa wengi kiasi hicho katika sekta ya afya kwa masomo hivi sasa jumla ya vijana 22.

Juzi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliwaaga pale vijana saba kwenda nchini Cuba na naamini tayari wameshaanza kozi hizo. Lakini wote jumla ya vijaa 22 sasa hivi naongelea *Master Degree ya Medicine* yaani *specialization* hivi sasa wapo Alexandria, wapo Cuba, wapo sehemu mbali mbali pamoja na Muhimbili Dar-es-Salaam wanaochukua masomo. Kwa hivyo, wakimaliza wote hao na wengine tunatarajia kupeleka tisa hivi karibuni tutafikia kiwango cha kutosha cha wataalam, lakini tuataendelea kushirikiana na vyuo vikuu vya wenzetu mbali mbali duniani ili kuweza kutoa elimu hiyo aliyouliza Mhe. Ali Suleiman Ali hapa *SUZA* namshukuru sana kwa swali lake zuri sana.

**Mhe. Spika:**Waheshimiwa Wajumbe maswali yetu yamekwisha, lakini kabla sijamwita Katibu kutupa taarifa, nitaomba niwape wajumbe wawili nitaanza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kanuni ya 42 halafu atafuatia Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kusimama kwa kanuni ya 42 ibara ya tisa sitaki Baraza liijadili *just* nataka tamko la serikali. Shida yangu kubwa au kadhia kubwa niliyosimamia kuhusu *ATM* za *PBZ* imekuwa na changamoto za kutosha hususan kipindi hiki cha mwisho wa mwezi hazifanyi kazi. Ndio maana hata hiyo hapo ya nje leo siku ya nne haifanyi kazi *ATM* ile inawapa usumbufu wananchi wetu juu ya upatikanaji wa fedha zao. Je, serikali inatoa tamko gani katika kadhia hii kuweza kuona kwamba zile *ATM* zina matatizo gani. Kwa sababu ukichukua *ATM* hizi na *ATM* za mashirika mengine zinafanya vizuri. Kwa hivyo, naomba tamko la serikali katika hilo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais au Mhe. Waziri wa Fedha naona yupo.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, naomba nijibu kama ifutavyo. Kwamba kwa vile taarifa hii ndio naipata sasa hivi kwamba *ATM* hizi zina matatizo naomba nilichukue suala hili nilifuatilie na *inshaallah* litapata ufumbuzi wake.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Waziri wa Fedha sasa namwita Mhe. Jaku Hashim Ayoub halafu naomba uongee taratibu kidogo ili tukusikie.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana na mimi nitazungumza kidogo kidogo muweze kusikia. Kwanza nikushukuru sana Mhe. Spika, kuniruhusu kusimama sijui kanuni ya 42 sijui utaniruhusu au itakuwa inajulikana imekuwa maarufu.

**Mhe. Spika:** Nafikiri tunaielewa lete hoja yako.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, kwa huzuni kubwa na kwa unyonge mkubwa nimesimama leo karibu mara ya nne katika kikao hiki kwa suala hili ninalosimamia kuhusu ngazi maarufu inaitwa *lift* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, mara nne kiti chako kinanieleza au jawabu

ninalolipata hapo kuwa serikali imechukua suala hili na jawabu utapata. Lakini leo Mwenyezi Mungu akijaalia Baraza linafungwa panapo uhai, kwa hiyo nimesimama na hoja yangu hii naomba uniruhusu niisome kidogo maana yake nimejipanga vizuri kwa suala hili na Baraza linavunjwa leo sijapata kauli naomba tujadili jambo la dharura.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na kilio cha ubovu wa ngazi ya umeme maarufu *lift* kwa lugha ya kitaalam katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo kwa mujibu wa sheria Nam. 3 ya mwaka 2016 ndio Hospitali ya Rufaa kwa hapa Zanzibar na ambayo ni kimbilio la wananchi wengi wanyonge ambao hawana uwezo kujitibu pahala pengine.

Hii sheria naomba niirudie tena mara ya pili, Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2016 ndiyo Hospitali ya Rufaa tumepitisha sisi. Ngazi ya umeme ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni muhimu sana kwa miundombinu ya hospitali hiyo kwa sababu baadhi ya huduma muhimu zinapatikana katika ghorofa ya juu kama vile uchunguzi, upasuaji na wagonjwa wa uangalizi wa karibu yaani *Intensive Care Unit (ICU)* kwa jina la kitaalam na wodi. Hivyo, kufikia huduma hizo kwa urahisi hasa na wagonjwa ni jambo muhimu katika hospitali hiyo na lazima iwepo ngazi ya umeme au *lift* kutoa huduma hiyo. Ngazi za umeme zote mbili zilizopo hivi sasa katika hospitali hiyo ni mbovu na zimepata maharibiko mara kadhaa. Hakuna athari ya ngazi hizo za umeme zikiachiwa kuleta athari kubwa kwa wananchi wanyonge wanaotafuta huduma za matibabu katika hospitali hiyo.

Tayari ngazi hizo zimeshawahi kuleta athari katika kutaka kusababisha kifo mwezi wa Disemba, baada ya umeme kukatika Hospitali ya Mnazi Mmoja mwananchi mmoja alikuwa mama nafikiri alijifungua watoto wawili kunasa kwa masaa kadhaa na ikafika kuzimia. Ilileta hofu na taharuki kubwa kwa wananchi wanaotafuta huduma katika hospitali hiyo. Kwa kuwa ngazi za umeme za hospitali hiyo zinaonekana kuwa zimeshapitwa na muda wake na hazifanyi kazi na hazifanyiwi matengenezo mara kwa mara ili kuziweka katika hali nzuri. Kwa vile hivi sasa kumekuwa na teknolojia mpya ya ngazi za umeme ambazo zinaweza kuhimili katika umeme ukikatika, ile *lift* inaweza ikafika pahala ikasimama wenyewe na ukaweza kuteremka. *Lift* ile ya Mnazi Mmoja imeshapitwa na wakati kwa kweli.

Mhe. Spika, umezimwa umeme ile *lift* ikafika pahala inakwenda wenyewe na inajifungua mlango wenyewe, lakini ile ni hatari kubwa tumeshuhudia wenyewe.

**Mhe. Spika:** Umeshafahamika Mhe. Jaku Hashim Ayoub nafikiri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Namalizia dakika moja kidogo Mhe. Spika. Madhumuni makubwa ya hoja yangu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna udhaifu au serikali yetu ina udhaifu, bali kutekeleza wajibu wangu kama Mwakilishi kukisaidia Chama changu cha Mapinduzi na juhudi za Mwenyekiti wetu ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hoja yangu ni hiyo.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nina maazimio matatu tu kuiomba serikali.

1) Serikali itenge fedha za bajeti kiasi cha shilingi milioni mia nne kwa mwaka huu tunaokwenda nao katika bajeti. *Lift* mbili zile karibu moja milioni mia moja na hamsini,

sawa sawa na gari ya waziri anayopanda mmoja, gari mpya hizi zilizotoka. Tukipata gari mbili tunaweza tukapata *lift* mbili.

Hoja yangu kubwa kikao kinachokuja cha bajeti sio kwenda kuzifanyia matengenezo *lift* zile zimeshatengenezwa na zimeshachoka. Serikali ambayo ni makini milioni mia nne zitengwe katika bajeti inayokuja, ndio hoja yangu kubwa na serikali haijashindwa kutenga milioni mia nne. Nimuombe Waziri wa Fedha, Wizara ya Fedha itakapokuja itenge milioni mia nne katika bajeti ya Wizara ya Afya. Kwa kuzikarabati vile itakuwa ni mtihani, kitakuwa kichwa hiki hiki tunakibadilisha kofia tu lakini bado matatizo yapo, au itakuwa kama njia ya Makunduchi zamani unaziba shimo hili ukifika mbele linazibuka tena jengine nyuma.

**Mhe. Spika:** Umeshamaliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kwa hivyo niombe:

2) Baada ya ununuzi wa ngazi hizo za umeme itoe ahadi kila mwaka kutenga fedha kiasi za kutosha kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ngazi za umeme za 2 Hospitali ya Mnazi Mmoja ili ziweze kuwa katika hali nzuri.

3) Wajumbe wa Baraza hili kupitia Kamati husika kusimamia upatikanaji wa fedha hizi mwaka 2018/19 atakayebahatika kuwa katika kamati hii. Ahsante Mhe. Spika.

Ahsante Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kujadili jambo hili.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante sana, nashukuru sana Mhe. Spika. *Bismillahi Rahmani Rahiym.* Naomba nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Paje kwa uchungu wake aliokuwa nao kwa wananchi, lakini uchungu ambao anaungana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo ina uchungu na wananchi wake pia sana hivyo hivyo kama yeye au kuliko yeye wakati mwengine.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba bado Baraza halijafungwa kauli ya serikali ya mwisho kabisa inatolewa na Mkuu wetu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado hajasoma hotuba yake. Kwa hivyo, bado fursa ya kupatikana kauli ya serikali tofauti na alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub ipo bado na nafasi ipo mpaka pale tutakapoakhirisha na wimbo wa taifa utakapopigwa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, mimi nitapenda kutoa maelezo ya ziada kwa hayo maazimio matatu hatutaki kwenda kuyafanyia kazi maana haya tayari yanafanyiwa kazi na serikali inaweza hapa hapa kutoa kauli yake. Sote sisi ni sehemu ya serikali na mkuu wetu ni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Mnadhimu wetu Mkuu panapokuwa na jambo lolote Mhe. Mohammed bin Aboud, Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, na leo serikali ipo kamili hapa na Manaibu Waziri wote wapo kamili.

Mhe. Spika, naomba nimuombe sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa heshima kabisa na taadhima hili suala tayari serikali inalifanyia kazi. Jana katika muelekeo aliokuwa akisoma Mhe. Waziri wa Fedha alisoma vizuri sana vipaumbele ambavyo tunamshukuru tena Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, vipaumbele viwili kavipa *priority* nzito zaidi, elimu na afya kwa wananchi wa Zanzibar.

Hata ile bajeti wakati inagaiwa basi sehemu hizo mbili kazipa vipaumbele vya kwanza kabisa, halafu ndiyo wengine wote wanafuatia. Hii ni kwa sababu ya uchungu wake, mapenzi yake na upendo wake yeye pamoja na serikali yake kwa wananchi wa Zanzibar. Wizara ya Afya mwaka huu wa fedha tutakaoishia Juni sisi tutakuwa kwenye bajeti yetu kiasi cha bilioni sabini, hatuwezi kushindwa na milioni mia nne, mia mbili, mia tano haiwezekani.

Mhe. Spika, jana Mhe. Waziri wa Fedha wakati anasoma muelekeo wake ametaja *more than one trillion* kama mtakumbuka muelekeo wa huko tunakokwenda, kwa hivyo naamini tutakapofika wakati bajeti zetu zote sisi wizara zitakuwa zimeongezeka na mapato Mwenyezi Mungu akitujaalia atatutilia baraka yatakuwa yameongezeka. Nimuombe Mhe. Jaku Hashim Ayoub hili suala la *lift* litatengewa bajeti yake maalum katika huu muelekeo tunaokwenda nao na itapata fedha ya kubadilishwa mifumo yake mingine.

Mhe. Spika, la pili pia naomba nitoe taarifa kwamba katika mradi ule wa *Kuwait Fund, BADEA* na *Saudi Fund,* suala la *lift* umo katika *feasibility study,* kwa hiyo mikataba ile ambayo imeshasainiwa kazi ile itakapoanza pia suala la *lift* limo mle ndani. Lakini sisi hatutosubiri mikataba hiyo ya *Kuwait Fund, Saudi Fund* na *BADEA,* sisi pia tutafanya jitihada maalum katika huo muelekeo uliotajwa jana wa kutenga bajeti yetu katika kipindi hiki.

Lakini jengine ili wananchi wasiendelee kupata shida tayari tumeshafanya mawasiliano mazuri sana na wenzetu wa Wizara ya Fedha wametenga fedha za kutengeneza katika kipindi hiki cha mpito kuelekea kwenye bajeti, ili wananchi kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wengine kama Mhe. Abdalla Ali Kombo asipate shida ya kupandishwa wakiwa na matatizo yoyote. Mwenyezi Mungu awaepushie maradhi yote, wawe na afya njema *inshaallah* wasihitaji huduma hizo. Kipindi hiki cha mpito Mhe. Spika, tunatarajia kufanyika matengenezo, lakini kipindi kinachokuja tayari bajeti itatengwa kwa ajili ya hilo.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa naomba niwapongeze Wajumbe wa Kamati alitaja suala la kamati wasimamie tayari. Naomba nimjulishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub chini ya usimamizi mahiri wa Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na kamati yeti nzima, Mjumbe mmoja leo aliuliza swali hapa Mhe. Hidaya Ali Makame yale ni muelezo wa kusimamia, hili jambo wamelisimamia kwenye kamati, wameshatwambia mara kadhaa wamekuwa wakilisimamia na tunaendelea nalo. Katika kamati nyengine iliyoundwa ya Chama cha Mapinduzi, chama kinachotawala ambaye Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni Mjumbe rasmi katika Kamati hiyo ya Chama cha Mapinduzi, *Caucus* ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi nayo pia suala la *lift* nimelitaja. Tumeshakaa na wetendaji wetu, tumeshakaa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, tumeshakaa na Waziri wa Fedha wote wanatoa mashirikiano mazuri sana katika hii *stage* tuliyokuwa nayo katika kutafuta fedha tumekubali sisi wenyewe kukatwa sehemu nyengine ili fedha hizo ziingizwe kwenye suala la *lift*.

Namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub atukubalie tayari kampuni husika imeshaleta mikataba yao, wameshaleta *quotation* yao ya matengenezo pamoja na mfumo mzima. Kama yeye atakuwa na taarifa zote za ziada sisi tupo tayari kushirikiana na yeye, watu laini kabisa, watu wepesi kabisa, atuletee hizo taarifa tushirikiane pamoja. Kwa sababu mwisho wa siku nyumba yetu tunayoijenga ni hii moja, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Zanzibar kuwatumikia wananchi wake kutokana na ahadi zilizochukuliwa na Ilani hiyo ya Chama cha Mapunduzi wakati Rais Dkt. Ali Mohamed Shein akiomba ridhaa ya wananchi wampe miaka mitano ya

kuongoza na sisi *Alhamdulillah* ndiyo tunaomsaidia tumechaguliwa wengine Mawaziri, wengine watendaji mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba tena niombe hili kweli linaletwa takriban mara ya sita kila siku suala la *lift, lift,* hata huko tukitoka nje wananchi pia wamekuwa wakituuliza suala hili kwa sababu ya hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Naomba ikubalike kwamba yeye ameshafanya kazi yake vizuri Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa wananchi wa Zanzibar, wamemuona na limefahamika na sisi pia tumelipokea tunakwenda kulifanyia kazi na kazi hii sio kwamba tunaianza sasa hivi, tayari tumeshaianza na inaendelea.

Mhe. Spika, hiyo ndio kauli ya serikali na kauli nyengine ya mwisho kabisa kabisa itatolewa na kauli nyengine ya mwisho kabisa itatolewa na Mkuu wetu wa Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nadhani tutakuwa tumefikia pahala mimi kama Spika nimeridhika na haya ambayo Mhe. Waziri ameyazungumza. Kwa hivyo, naomba na wewe uwe umefahamu, umeridhika kiasi hicho. Lakini kama bado hujaridhika basi naomba ukutane na Mhe. Waziri umpe hizo *details* ambazo unazo ili liweze kuharakishwa hili jambo.

Lakini pia Mhe. Waziri amegusia huenda tukasikia kitu kwenye hotuba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo basi, tustahamili tusikilize hicho kilichomo, lakini kama pia bado utakuwa hujaridhika bado unayo nafasi Mheshimiwa kuwatumikia wananchi nje ya Baraza sio lazima ufanye kazi ukiwemo humu ndani, lakini nje ya Baraza unaweza ukamfuata Mhe. Waziri na mkaweza kulifikisha pahala hili. Ahsante sana kwa bidii yako Mheshimiwa nakushukuru sana naomba tuendelee.

Naomba nitoe tangazo kwanza. Kwanza kabisa naomba niikumbushe serikali kulikuwa kuna majibu ambayo alitakiwa apewe Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kuhusiana na ajira za Arabuni, lakini mpaka tunafunga sasa hivi jibu hilo alikuwa bado hajalipata. Naomba nikukumbusheni tu ili baadae mnaweza kutafuta namna ya kuweza kumpa haya majibu Mheshimiwa au mkasubiri kwenye kikao kinachokuja mkayaleta rasmi hapa Barazani. Baada ya hapo naomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kwamba mara baada ya kuwasilisha Shughuli za Baraza tutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi, mara tu baada ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuakhirisha Baraza.

Lakini pia nimepata taarifa ya mazoezi, Mwenyikiti wa *Baraza la Wawakilishi Sports Club,* Mhe. Hamza Hassan Juma, anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na wapenzi na wachezaji wa Baraza la Wawakilishi kuhudhuria katika mazoezi yatakayoanza siku ya Alkhamis tarehe 8/3/2018 kwa utaratibu ufuatao:

Wanaume *football* Uwanja wa Wazee Maisara, wanawake *netball* viwanja vya Baraza la Wawakilishi Chukwani. Mazoezi yatafanyika siku ya Alkhamis, Ijumaa na Jumamosi kuanzia saa 12:00 hadi saa 2:00 za asubuhi. Shime tuhudhurie kwa wingi ikiwa ni njia moja ya kuimarisha afya zetu pamoja na kujiandaa kwa ajili ya michezo ya Pasaka. Shukrani sana.

Waheshimiwa Wajumbe, Ahsante sasa naomba nichukue nafasi hii kwa heshima na taadhima nimkaribishe Mhe. Mkamu wa Pili wa Rais ili aje atufungie Baraza. Mheshimiwa karibu sana.

## KUAKHIRISHA BARAZA

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza kabisa, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehma, mwenye kuneemesha neema zote hapa ulimwenguni na kesho Akhera, kwa kutujaalia hali ya uzima na afya njema ambayo imetuwezesha kuwepo hapa wakati huu baada ya kufanikisha vizuri Mkutano wa Tisa wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi ulioanza tarehe 07 Febuari, 2018. Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya Mkutano huu zimekamilika kwa wakati na kwa ufanisi wa kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma pamoja na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuviendesha vyema vikao vyetu kwa hekima, busara na weledi mkubwa na kukifanya kikao hiki kumalizika kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, kwa umuhimu na uzito wa kipekee nampongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuisimamia vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Chama chetu cha Mapinduzi (CCM). Usimamizi wake huo umetuletea mafanikio ya kupigiwa mfano ambayo tunajivunia na kutufanya twende kifua mbele.

Mhe. Spika, nampongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kukamilisha ziara yake ya nchi ya Falme za Kiarabu. Safari ambayo italeta manufaa makubwa ya kuinua uchumi wa nchi yetu ikiwemo masuala ya utafiti na uchimbaji wa mafuta, Sekta ya Utalii, Sekta ya Biashara, Sekta ya Afya, ushirikiano wa kidiplomasia, uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo pamoja na ujenzi wa barabara. Lakini pia, ziara hiyo imeimarisha uhusiano wetu mzuri uliopo baina ya Zanzibar na *UAE*. Mapokezi aliyoyapata yanadhihirisha kuimarika huko kwa uhusiano wetu huo.

Mhe. Spika, katika kuimarisha na kuhamasisha michezo nchini, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ametimiza ahadi yake aliyoitoa kwa wanamichezo wetu na kuwapa zawadi mbali mbali wanamichezo wetu wa Timu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes* na *Sand Beach Heroes* kwa kila mchezaji na viongozi wa timu hizo kwa juhudi na moyo waliouonesha kwa kuipatia sifa nchi yetu na kufungua ukurasa mpya katika tasnia ya michezo katika ramani ya dunia.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kumteua Ndg. Mohammed Hassan Haji kuwa Kamishna wa Polisi Zanzibar. Uteuzi huo unaonesha imani ya Mhe. Rais aliyonayo kwa utendaji wake wa kazi. Ninaamini kwamba Kamishna Haji ataendelea kuliimarisha Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu ya ulinzi wa raia na mali zao hapa Zanzibar kwa uadilifu na umakini mkubwa pamoja na kuitunza amani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kadhalika tunakipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 41 tokea kuzaliwa kwake mwaka 1977 kwa mafanikio makubwa sana. Chama hiki kimeweza kuisimamia

amani, umoja, utulivu na mshikamano katika nchi yetu na kuendelea kutoa maelekezo na miongozo kwa viongozi na watendaji mbali mbali wa serikali na kuleta ufanisi katika utendaji wetu wa kazi za kuwatumikia wananchi wetu. Tunaamini kwamba, miongozo na maelekezo hayo yanasaidia sana katika kuongeza uweledi na uwajibikaji unaotoa mchango mkubwa wenye kuleta maendeleo endelevu nchini.

Mhe. Spika**,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekamilisha na kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wake wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020 kwa muda wa miaka miwili kuanzia mwezi Oktoba, 2015 hadi Septemba, 2017 na kuwasilishwa katika Mkutano Mkuu wa CCM unaofanyika mwezi Disemba, 2017 huko Mkoani Dodoma. Taarifa hiyo imeonesha utekelezaji halisi wa maagizo ya ilani yetu na tayari karibu asilimia 60 ya maagizo hayo yamekamilika utekelezaji wake. Nazisihi Taasisi zote za Serikali kuendelea na utekelezaji wa maagizo yaliyobakia kwa kufuata taratibu na miongozo inavyotuelekeza.

Mhe. Spika**,** nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kusimamia vyema utekelezaji wake na nawaomba waendelee na juhudi hizo ili lengo la serikali likamilike kwa wakati. Ofisi yangu itaendelea kuziratibu Taasisi za Serikali ili kuhakikisha utekelezaji wa ilani unafikia asilimia 100 ifikapo 2020.

Mhe. Spika**,** katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, serikali inaendelea kuchukua hatua kali za kisheria juu ya wote watakaobainika kushiriki katika kadhia hii ikiwemo wafanyakazi na wale wote wanaoshiriki katika kuwalinda na kuwakingia kifua wahalifu wa udhalilishaji. Aidha, serikali haitamvumilia wala kumuonea aibu wala muhali mtu yeyote wa cheo chochote na ngazi yoyote pindi akibainika kutenda jambo hilo. Waheshimiwa inatupasa tutambue kwamba "Sheria ni Msumeno".

Mhe. Spika**,** navisihi vyombo vya ulinzi na usalama kupambana zaidi juu ya mambo hayo yanayoitia aibu nchi yetu pamoja na kuharibu maisha ya wananchi wetu. Ni wajibu wa jamii kutoa ushirikiano wa kutosha ili kukabiliana na tatizo hilo, kwa kuwafichua na kutoa taarifa za matukio hayo, kutozimaliza kesi hizi majumbani. Nawasihi wahusika kufika mahakamani na kutoa ushahidi ili sheria iweze kuchukua mkondo wake na haki iweze kutendeka na hatimae kuvimaliza vitendo hivi katika nchi yetu.

Mhe. Spika**,** tayari Baraza lako Tukufu limekwishapitisha sheria ya adhabu. Sheria ambayo imeweka bayana kuwa mtuhumiwa yeyote wa kosa la udhalilishaji hatopaswa kupewa dhamana. Sheria hiyo sasa inangojea kuwekwa saini na Mhe. Rais tu ili iwe sheria ambapo Mhe. Rais ataifanya kazi hiyo baada ya muda sio mrefu.

Mhe. Spika**,** katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Serikali kupitia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imeendelea na juhudi mbali mbali ikiwemo kutoa taaluma za athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa makundi ya kijamii zikiwemo skuli 446 za Msingi na Sekondari, ambapo tayari Tume imewafikia wanafunzi 54,532. Tume pia imetoa taaluma katika Vyuo vya Elimu ya Juu, maeneo mbali mbali ya kazi pamoja na Vikosi vya Ulinzi na Usalama. Kadhalika, Tume imeandaa na kurusha vipindi 456 vya taaluma. Aidha, Serikali inaendelea kuzisaidia nyumba za upataji nafuu kwa vijana walioamua kwa hiari zao kuacha matumizi ya dawa za kulevya. Katika mwaka 2017 jumla ya vijana 370 wameweza kupatiwa huduma katika vituo hivyo Unguja na Pemba.

Mhe. Spika**,** napenda kuwahimiza Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu na Viongozi wengine katika ngazi mbali mbali kuunga mkono juhudi za kupambana na dawa za kulevya kwa kuwaelimisha wazee na jamii nzima kwa ujumla kuondoa unyanyapaa kwa vijana ambao wameamua kwa hiari zao kuacha dawa za kulevya. Na tuwe tayari kuwapokea na kuishi nao vijana wetu ili wajihisi kuwa ni sehemu ya jamii na wanathaminiwa na sio kuwavunja moyo na kuwakatisha tamaa. Tuwaoneshe vijana hao kuwa hawatengwi tena na jamii.

Mhe. Spika**,** suala la upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini limekuwa likishughulikiwa ipasavyo na serikali yetu. Katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi serikali imejipanga kutekeleza miradi mikubwa minne ifuatayo:

i. Mradi wa kwanza ni wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Afrika wa Awamu ya 12 *(ADF 12).*

   Mradi huu unatarajia kubadilisha mabomba machakavu na kuweka mabomba mapya yenye urefu wa kilomita 68 katika maeneo ya Bumbwisudi, Kinumoshi, Kianga, Welezo, Mwembe Mchomeke, Amani, Kiponda na Mji Mkongwe; na kujenga matangi 2, Saateni 1 na Mnara wa mbao 1. Utekelezaji wa mradi huu tayari umeshaanza na unatarajiwa kugharimu jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 48 hadi kukamilika kwake.

*ii*. Mhe. Spika, Mradi wa pili ni kuimarisha Miundombinu ya Maji Mjini unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA).*

   Mradi huu utatekelezwa kwa ujenzi wa matangi katika maeneo ya Welezo Juu, Welezo Magharibi na Zoni ya Migombani kwa ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 120 na uwekaji wa umeme katika maeneo husika ya utekelezaji wa mradi huu ambao unatarajiwa kugharimu jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 225.

iii. Mhe. Spika, Mradi wa tatu ni Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mjini unaofadhiliwa na Serikali ya India. Huu ni mradi mpya utakaohusisha ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Zoni ya Mfenesini, Kizimbani, Tunguu na Fumba kwa kuchimba visima, kuweka mabomba ya kuvutia maji pamoja na kuvuta umeme katika maeneo ya visima vitakavyo chimbwa. Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 207 hadi kukamilika kwake; na

iv. Mradi wa nne ni Uchimbaji wa Visima na Usambazaji wa Maji Vijijini unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mradi huu unahusisha uchimbaji wa visima 11 katika maeneo ya Chaani, Donge, Kisongoni, Kiboje na Miwani; pamoja na ujenzi wa matangi 3, Kisongoni 1, Kiboje 1 na Miwani 1; pia ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 20.178 katika maeneo ya Kiboje na Miwani na uvutaji wa umeme. Mradi huu unatarajiwa kugharimu Shilingi za Kitanzania Bilioni 12 hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika**,** ili miradi hiyo yote iwe endelevu, tunawaomba wananchi waondokane na dhana ya uchangiaji wa maji kuwa ni jukumu la serikali pekee. Kwa maana hiyo, tunawaomba wananchi kuchangia gharama za huduma hizo kwa wale wote wanaopata huduma hiyo.

Mhe. Spika**,** kwa kuzingatia miradi hiyo na gharama zake, mkopo wa Shilingi Milioni 200 uliopendekezwa kutolewa kwa serikali kwa njia ya mkopo usingefaa kwa chochote wala lolote.

Mhe. Spika**,** hivi karibuni kumekuwepo na upungufu wa mafuta nchini ambao umeathiri shughuli za kiuchumi. Upungufu huo umesababishwa na kuwepo na foleni kubwa ya upakizi katika bandari ya Dar-es-Salaam pamoja na kuongezeka kwa idadi kubwa ya matumizi ya nishati hiyo kwa kiwango cha juu kutoka lita milioni 10 katika mwezi wa Disemba, 2017 hadi kufikia lita milioni 17 kwa mwezi wa Januari, 2018. Aidha, serikali ilikuwa inatumia mfumo wa uingizaji wa mafuta kwa pamoja *(BPS)* ambao ulituwezesha kujua idadi halisi ya matumizi ya mafuta Zanzibar kwa wakati huo pamoja na kudhibiti ubora wa mafuta unaoingizwa nchini, ambapo kwa sasa mfumo unaotumika ni kila kampuni kuingiza mafuta yake wenyewe au *multiple importation*.

Mhe. Spika**, s**erikali inalishughulikia suala la upungufu wa mafuta kwa umakini wa hali ya juu na imejipanga kuchukua hatua za muda mfupi, wa kati na mrefu ili suala la upungufu wa mafuta liwe historia nchini mwetu. Kwa taarifa zaidi zitaelezwa kwa undani katika bajeti ijayo. Hivyo, natoa wito kwa wananchi kuwa wastahamilivu na sio nia ya serikali kuwapa wananchi wetu usumbufu. Serikali inalitambua suala hilo inakereka nalo na haifurahii kuwepo kwa tatizo hili hapa nchini na iko mbioni kulimaliza suala hili lisitokee tena.

Mhe. Spika**,** kuhusu suala la ulipaji umeme kwa deni la *TANESCO* kwa upande wa Zanzibar, serikali iliamuru Shirika la Umeme *(ZECO)* lilipe deni la umeme kwa *TANESCO* kwa kiwango cha Shilingi Bilioni mbili kila mwezi na Wizara ya Fedha kulipa deni hilo kwa kiwango cha TZS Bilioni moja kila mwezi, Shirika la Umeme na Wizara ya Fedha walianza utekelezaji huo.

Katika utekelezaji huo changamoto zimejitokeza kwa upande wa Shirika la Umeme *(ZECO)* kwa kutoweza kuendelea kulipa kwa ukamilifu kiwango kilichoagizwa na serikali cha shilingi bilioni mbili kila mwezi. *ZECO* imeweza kulipa deni hilo kwa kiwango kilichoagizwa na serikali kwa kipindi cha miezi minne (4) kuanzia Juni, 2017 hadi Oktoba, 2017, miezi mingine iliyobakia ililipa deni hilo chini ya kiwango kilichoagizwa na serikali.

Mhe. Spika**,** kutoweza kutimiza agizo hilo ni kutokana na changamoto ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ankara za matumizi ya umeme kutoka kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za Muungano zilizopo Zanzibar, ambapo inapelekea kutokuwa na mapato ya kutosha kulipa deni hilo kila mwezi kama ilivyoagizwa na serikali baada ya kukidhi mahitaji mengine ya msingi ya kuliendesha shirika hilo.

Mhe. Spika**,** kuhusu ulipaji wa ankara za matumizi ya umeme kwa Taasisi za Serikali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliagiza Wizara ya Fedha kulipa deni la ankara za matumizi ya umeme kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi mwezi wa April, 2017. Pia, kuanzia mwezi wa Mei, 2017 Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ziliagizwa kuendelea kulipa ankara za matumizi yao ya umeme ya kila mwezi, naamini taasisi hizo zimeendelea kufanya hivyo.

Mhe. Spika**,** Viongozi wetu Wakuu Wastaafu wameitumikia nchi yetu na watu wake kwa juhudi, maarifa, uweledi na mapenzi makubwa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitenga fedha maalum katika bajeti yake ili kuwaenzi na kuwahudumia viongozi wake hao kwa mujibu wa sheria na hakuna hata kiongozi mmoja miongoni mwao aliyewahi kulalamika kwa kukoseshwa huduma wanazostahiki kwa mujibu wa sheria. Nakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi kufanya uchunguzi wa kina kabla ya kutoa hoja zenu za kuchangia mijadala katika Baraza lako Tukufu. Sio busara wala haikubaliki kutoa hoja kwa ajili ya kujijengea umaarufu bila ya kuchunguza na kuthibitisha ukweli wa hoja inayotolewa. Hii itasaidia sana kuondoa mizozo na migongano miongoni mwa wananchi na kuifanya mijadala hiyo kutokuwa na tija.

Mhe. Spika, suala la kupunguza umaskini ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali yetu. Serikali kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini *TASAF* awamu ya tatu, kwa mwezi wa Januari – Februari, 2018 imelipa jumla ya shilingi bilioni 1,096,244,000/ kwa walengwa 30,543 Unguja na Pemba. Hivi sasa walengwa wa mpango huo wanaendelea na kazi za ajira za muda Unguja na Pemba na hivyo kuwapunguzia ukali wa maisha.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kufuatilia kwa umakini utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo unaohusisha kusaidia miradi midogo midogo inayoibuliwa na wananchi katika majimbo yote ya Unguja na Pemba. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kufuata sheria zake na kufanya marejesho kwa wakati ili serikali iweze kukamilisha taratibu nyengine za mfuko huo. Serikali haitatoa fedha kwa jimbo lolote ambalo halitafanya marejesho ya matumizi ya fedha iliyotolewa awali.

Mhe. Spika, elimu ndio msingi mkubwa wa mafanikio yetu katika kukuza maendeleo na mustakbali wa nchi yetu na wananchi wake. Kwa kulitambua hilo, serikali inaendelea na ujenzi wa majengo mapya ya skuli pamoja na kufanya matengenezo kwa majengo yaliyochakaa Unguja na Pemba. Lengo ni kuwa na miundombinu iliyo bora na salama ambayo itapelekea kupata elimu bora na ya uhakika. Hivyo basi, natoa rai kwa walimu na wazazi kuwahamasisha watoto wasome kwa bidii pamoja kusimamia malezi yaliyo bora kwa watoto wetu ikiwa ni pamoja na kuzingatia mila, utamaduni na silka zetu, hususan katika kipindi hiki cha utandawazi. Vile vile, serikali inaahidi kusimamia zaidi suala la elimu ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya kukalia, maabara na vitabu vya kiada na ziada ili kuwa na matokeo mazuri katika mitihani yao.

Mhe. Spika, serikali ina jukumu la msingi la kuhakikisha huduma za afya zinatolewa na kupatikana na wananchi wote. Kutokana na hali hiyo, serikali inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma hiyo mijini na vijijini. Pamoja na hayo, serikali inatumia fedha nyingi ili kuwanusuru wananchi wake kukabiliana na maradhi ya aina mbali mbali ikiwemo maradhi ya malaria pamoja na maradhi mengine yasiyoambukiza, kama vile sukari. *pressure* na kadhalika.

Mhe. Spika, kinachosikitisha ni kuona baadhi ya wananchi wanakataa kupigiwa dawa za mbu na vidudu vingine vinavyoweza kusababisha maradhi na wataalam wetu. Ninawaomba wananchi waachane na tabia hizo pamoja na imani walizonazo juu ya dawa hizo. Serikali inawajali na inatambua umuhimu wa kazi hiyo kwa mustakabali wa watu wake na haipo tayari kuona jamii inakumbwa na matatizo. Ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wawasimamie wananchi katika majimbo yao ili wakubali nyumba zao kupigiwa dawa na kujiepusha na maradhi yanayosababishwa na mbu.

Mhe. Spika, katika kuimarisha makaazi na kuweka mandhari nzuri ya Mji wetu wa Zanzibar, serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - Zanzibar inaendelea na ujenzi wa nyumba za makaazi katika eneo la Mbweni Zanzibar ambao umeanza mwezi Novemba, 2015. Mradi huu utakuwa na majengo 18 na kila jengo litakuwa na ghorofa 4 yenye nyumba 14. Ifikapo mwishoni mwa mwezi wa Machi, mwaka huu tunategemea kukabidhiwa majengo matano (5) ambayo ni sawa na nyumba 70. Napenda kuchukua nafasi hii kuwataka wananchi kujitokeza kununua au kukodi nyumba hizi za *ZSSF* ambazo ni za bei nafuu.

Mhe. Spika, serikali imeanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanda Vikubwa, vya Kati na Vidogo Vidogo ikiwa na madhumuni ya kukuza uchumi wa nchi, ajira na kuongeza kipato cha mtu binafsi. Kwa muktadha huu, serikali inawaomba na kuwataka wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika sekta hii muhimu ili kufikia katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda. Viwanda vitasaidia sana uchumi wa nchi na pia vitasaidia upatikanaji wa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, katika kipindi kijacho tunategemea kupata mvua za masika ambazo zina manufaa makubwa sana kwa nchi yetu. Nawaomba wakulima watumie vizuri mvua hizo kwa kuotesha mazao ya chakula na biashara kwani ni njia moja muhimu sana ya kuongeza vipato vyetu na kuondokana na umaskini. Hata hivyo, tunawasihi wale ambao bado wanakaa katika njia za maji na mabondeni kuchukua tahadhari kubwa sana juu ya ujio wa mvua hizo, kwani nchi yetu ilikumbwa na majanga yatokanayo na mvua yakiwemo mafuriko katika kipindi kilichopita. Mafuriko yaliyosababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Mamlaka husika zitaendelea kutoa tahadhari na tunapaswa kuchukua hatua kukabiliana na hali hiyo.

Mhe. Spika, katika mkutano wetu huu wa tisa jumla ya maswali ya msingi 71 na maswali ya nyongeza 206 yaliulizwa na yalijibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Nawashukuru sana Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kutoa majibu ya ufasaha na ya kina katika maswali hayo. Mkutano wetu pia, umejadili kwa kina miswada mitatu muhimu ambayo ni:

i) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo;

ii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu na kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo; na

iii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, miswada yote hii ilichangiwa kwa kina na sasa tayari tumeshaipitisha kuwa sheria ambazo zitatuwekea utaratibu ulio bora zaidi wa kushughulikia kero za wananchi wetu katika maeneo ya biashara na utoaji wa haki. Kwa kuwa miswada hii ilijadiliwa vya kutosha sina haja ya kuongeza jambo lolote. Hata hivyo, napenda mtambue kwamba, sheria hizi hazitafanya kazi

vizuri kama hazitotungiwa kanuni baada ya kupitishwa kama tulivyokumbushwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo, na kusisitizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu. Hivyo, nawasihi mawaziri wote ambao bado hawajatunga kanuni ya sheria zinazohusika na sekta zao wafanye hivyo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kadhalika mkutano wetu huu ulipokea na kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza letu ambazo ni:-

1. Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Mwaka 2017/2018.
2. Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Mwaka 2017/2018.
3. Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Mwaka 2017/2018.
4. Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Mwaka 2017/2018.
5. Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2017/2018.
6. Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Mwaka 2017/2018.
7. Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) ya Mwaka 2017/2018 na
8. Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, vile vile Baraza lako Tukufu lilipokea na kujadili ripoti ya serikali kuhusu hoja binafsi ya mjumbe kuhusu kuweka miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu katika majengo, barabara, makaazi, maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine na Ripoti ya Serikali kuhusu maombi ya wananchi wa Kisakasaka Zanzibar kuhusu namna wanavyoweza kufaidika kutokana na machinjio ya wanyama yaliopo kwenye maeneo yao; pamoja na Ripoti ya Mapendekezo ya Muelekeo wa Mpango wa Taifa.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu ripoti zilizotolewa naomba uniruhusu kuzungumzia kidogo Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*). Serikali inaelewa wazi kuwa heshima yake mbele ya macho ya wananchi wake inategemea kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyoshughulikia wabadhirifu wa mali ya umma. Bila shaka, serikali yetu haitaifumbia macho Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*). Watumishi wote walioguswa na ripoti hii watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zetu. Serikali imekuwa ikifanya hivyo na itaendelea kufanya hivyo bila ya kumuonea mtu.

Mhe. Spika, ripoti zote hizi kwa jumla zinaonesha umahiri na kiu ya maendeleo waliyokuwa nayo wajumbe wako ya kuitaka nchi yetu iondoke hapa ilipo na ielekee kwenye maendeleo makubwa zaidi yanayojali maslahi ya wengi. Napenda kuwaahidi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi kuwa, mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe waliyoyatoa katika ripoti zote hizo yatafanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa umakini wao wa kuyatolea ufafanuzi wa kina maswali yote yaliyoulizwa. Nawaomba tuendelee kwa bidii kutekeleza na kusimamia kazi zetu ili kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kukupongeza wewe Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa kuliendesha vyema Baraza hili. Hekima na busara zenu

zimesaidia sana katika kuumaliza mkutano huu kwa salama. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kushiriki kikamilifu na kutoa michango na mapendekezo ya kuimarisha utendaji wa serikali. Nawaomba muendelee na moyo wa kuijali serikali na wananchi wake.

Mhe. Spika, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuchapa kazi na kushirikiana na serikali yao katika maendeleo ya kila siku. Kwa mara nyengine tena napenda kuvishukuru vyombo vyetu vya habari vyote vya serikali na binafsi, pamoja na wakalimani wetu wa lugha za alama kwa kazi zao nzuri za kuwajuvya wananchi wetu mambo yanayoendelea kwenye Baraza letu Tukufu.

Mhe. Spika, mwisho napenda kuwaombea Waheshimiwa Wajumbe safari njema ya kurejea kwenye vituo vyao salama ili wakawatumikie wananchi wao na kuwaletea maendeleo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa naomba kuchukua fursa hii kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 9 Mei, 2018 saa 3:00 barabara za asubuhi Mwenyezi Mungu akitujaalia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba ambayo umeitoa. Waheshimiwa pamoja na hotuba hiyo, Mheshimiwa ametoa hoja na imeungwa mkono kwamba tuliakhirishe Baraza letu mpaka siku ya Jumatano tarehe 09 Mei, 2018, saa 3:00 asubuhi. Sasa wale wote wanaounga mkono hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kutolewa hiyo hoja na ikapigiwa kura kwa maana ya kwamba imepita, sasa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe katika mchakato mzima huu wa uendeshaji wa Baraza kipindi hiki. Nimshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake, niwashukuru Mawaziri, niwashukuru na Wajumbe wote kwa pamoja changamoto mbali mbali ambazo zimejitokeza na namna ambavyo tumekabiliana nazo humu Barazani. Baada ya hapo naomba nichukue nafasi hii sasa kuliakhirisha Baraza la Wawakilishi hadi siku ya Jumatano tarehe 09 Mei, 2018 saa 3:00 barabara za asubuhi. Kwanza mnyanyuke kwa ajili ya wimbo wa taifa.

*(Saa 5:00 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi*
*tarehe 09/05/2018 saa 3:00 asubuhi)*

*WIMBO WA TAIFA*